

# CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

## KITIVO CHA SANA NA SAYANSI ZA JAMII

S. L. P 23409,  
Nukushi: 255-22-2668759,  
Dar es Salaam, Tanzania.  
<http://www.out.ac.tz>



Simu: 255-22-2666752/2668445  
Nukushi: 255-22-2668759,  
Baruapepe: [dfass@out.ac.tz](mailto:dfass@out.ac.tz)

11<sup>th</sup> Machi 2023.

Kwa mwanajumuia ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,

### **YAH: MWALIKO WA KUHUDHURIA WARSHA YA KUBADILISHANA UZOEFU KUHUSU WATOTO NA WATU WENYE ULEMAVU**

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo cha Ualimu Patandi, Chuo Kikuu cha Western University of Applied Science (Norway), and Chuo Kikuu cha Molde (Norway) wanendesha mradi wa kuwasaidia watoto na watu wenyе ulemavu. Mradi huu unadhaminiwa na Kituo cha Kimataifa cha Kubadilishana Umahiri cha Norway (NOREC) kama utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, kama vile Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC) na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenyе Ulemavu (CRPD).

Mpaka kufikia sasa, mradi umepata mafanikio, uzoefu, na maarifa faafu kwa jamii yetu na jamii zingine zinazoishi na watu wenyе ulemavu. Hivyo basi, tunapenda kukualika wewe mwanajumuia wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania **uliyeko Dar es Salaam** (uwe mwanafunzi, mfanyakazi muendeshaji au mwanataluma) katika warsha hii ya kubadilishana uzoefu. Uwepo wako utakuwezesha kusikiliza yale yaliyokwishafanyika na kukupa nafasi ya kutoa mchango wako ili kuboresha na kufanya mradi kuwa endelevu.

Warsha itafanyika tarehe 27 Machi 2024 hapa Makao Makuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuanzia saa 3 za asubuhi mpaka saa 8 za Mchana. Warsha itafanyika katika Jengo la Elimu Masafa (ODL Tower) orofa ya tano. **Endapo utachagua kushiriki, tafadhali jiorodheshe kwa kubonyeza kiungo kifuatacho kutuwezesha kupanga mipango mizuri ya kufanikisha ushiriki wako katika warsha.**

[https://docs.google.com/forms/d/e/1FAIpQLSfrJLP07vhScXcQpKqFPkwA6pv\\_Jfw7nMf11nZsRx1xauWg7A/viewform?usp=sharing](https://docs.google.com/forms/d/e/1FAIpQLSfrJLP07vhScXcQpKqFPkwA6pv_Jfw7nMf11nZsRx1xauWg7A/viewform?usp=sharing)

Mwisho natanguliza shukrani zangu za dhati kwa imani kubwa kwamba utaitikia wito huu wa kubadilishana Mawazo kwa manufaa ya ubinadamu na umma.

Wako katika ujenzi wa taifa,

Dr. Dunlop Ochieng,  
Mkuu wa Kitivo,  
Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii.